# KUZALIWA UPYA

*Mt. Yohana 3:1-8 Usistaajabu kwa sababu nilikuambia, Hamna budi kuzaliwa mara ya pili ……..*

Tunajua mbegu ya zamani lazima ife, kabla ya mbegu mpya haijatokea toka kwenye mbegu ya zamani, lazima ioze, hakika sio kufa tu lakini inaoza baada ya kufa.Tunafahamu hilo kwamba ni kweli. Hilo ni jambo lile lile ni sawa na kuzaliwa mara ya pili, kamwe haturudi nyuma, bali tunaendelea mbele wakati tunapozaliwa mara ya pili. Na ndiyo kwamba nafikiri leo tuko wengi – sio wengi hasa, waliozaliwa upya halisi; ni kwasababu mbegu ni – pengine watalionea huruma neno au mtu; lakini hawataki kuozea mbali toka kwa taratibu za asili hawataki kutoka humo wanataka wakae kwenye utaratibu wa zamani na wanadai kuzaliwa mara ya pili au wako kwenye ujumbe wa wakati wao.

Tumeliona hilo katika wakati wa Luther, Wesley Pentekoste na nyakati zote. Wanaendelea kujaribu kuishi katika mtindo wa zamani na wakidai hilo, lakini mtindo wa nyakati za zamani lazima ufe; uoze ilikutoa kilicho kipya. Bado wanataka kukikumbatia. Fahamu wanajua utaratibu wa zamani umekufa, lakini bado hawataki kuoza kutoka huo. Sasa, kuoza ni wakati umeachana nao kabisa.

Wakati wakifanya madai kwamba wamezaliwa upya……. lakini madai ni ishara tu ya kuzaliwa. Kuoza ndiko kunatoa kuzaliwa upya. Unapaswa kuozea mbali kutoka hiyo kama ilivyofanyika katika nyakati zote, kutoka wakati wa Wesley na wote waliofuata…… lakini kitu ni kwamba, baada ya uzazi mpya ni kutokea …… luther alikuja na ujumbe wa neno moja: mwenye haki ataishi kwa Imani (Rum 1:17). Vema, hakuweza kuukumbatia ule utaratibu wa zamani. Ilibidi atoke nje ya huo.

Na baadaye Watu wale waliegemea sana Neema (Kalvinist) waliliweka Kanisa Anglikana katika hali hiyo mbaya (kwenye mafundisho ya Kalvin) mpaka Mungu akainua mafundisho ya kisheria (ambayo yalikuwa ya John Wesley) ….. utaratibu wa zamani ulikufa ili kwamba utaratibu mpya utokee. Na wakati wa wesley ulipokoma na nyakati zote ndogo au majani yaliyotokea kwenye bua na kuchanua katika wakati wa Wesley …. Tazama wakati Pentecost ilipotokea kwa kurudishwa kwa vipawa, ilibidi watoke toka kwa Wabatist, Presbeyterian Pilgrin Holiness, Nazarine, kanisa la Kristo (lijiitalo) na yote hayo kwamba walitakiwa kutoka nje ya hilo, waoze mbali na hilo, na kukubali kuzaliwa mara ya pili.

Bila shaka yoyote, tupo katika wakati wa kanisa la Laodikia. Sasa mjumbe wake aliahidiwa katika Malaki 4:5-6. aliahidiwa kufanya hivyo, Na ujumbe wake ni kurudisha tena neno. Ni kurudisha watu kwenye neno, inabidi azaliwe kwenye uzazi mpya toka – kutokana na Malaki 4.

Vitu vyote vya asili vyaeleleza vya kiroho bila kujali je ulifahamu hilo? Vitu vyote vya asili vyaeleleza vitu vya kiroho. Kwa mfano kama huu, Tunapozaliwa katika mwili wa Kristo. Kuna vitu vitatu vinavyoleta kuzaliwa kwetu. Na hivyo ndivyo vitu vitatu vilivyotoka kwenye maisha uhai wa Yesu wakati alipokufa. Vilitoka kwenye mwili wake, maji, damu, Roho. Hivyo ni sahihi?

Vitu vitatu. Na vitu hivyo vitatu ndivyo tunapitia tunapozaliwa mara ya pili kuhesabiwa haki,kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, yote yanafanyika katika tendo moja, lakini inachukua … lakini unaweza kuhesabiwa mwenye haki pasipo kutakaswa. Lakini unaweza kumuamini Yesu Kristo na bado umebeba uchafu pamoja na wewe. Tena unaweza hakika ukaishi kwa Imani na maisha masafi na matakatifu bila Roho Mtakatifu.

Sasa tunafahamu pia kwamba Mungu amekamilishwa katika hali tatu. Sasa Mungu hukamilishwa katika hali tatu. Neema ni tano. Saba ni mwisho, kama Ulimwengu. Mungu hukamilishwa katika Baba, Mwana, na Roho Mtakakatifu. Huu ndio ukamilifu wa Mungu, vyote ni Mungu mmoja anajidhihirisha katika muonekano wa ofisi moja – au tatu katika Mungu mmoja. Sasa kuna mambo matatu katika ukamilifu wa hatua tatu za neema ndani ya Kanisa: Kuhesabiwa haki kwa Imani, kuna utakaso, na Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hivyo vinakamilisha kuzaliwa kwa pili. Kama vile tu kuzaliwa kwa asili kunavyolinganishwa na hilo. Ambapo Mwanamke anapozaa mtoto, kitu cha kwanza kutokea ni maji, damu, halafu uzima. Biblia ilisema katika Yoh. 5:7, “kuna watatu washuhudiao Mbinguni, watatu hawa ni mmoja kuna watatu washuhudiao duniani maji, damu na roho, hawa hupatana katika habari moja”.

Sasa Baba, Mwana na Roho Mtakatifu ni mmoja. Huwezi kuwa na baba bila kuwa na Mwana, pia huwezi kuwa na Mwana bila kuwa na Roho Mtakatifu. Lakini unaweza kuhesabiwa haki pasipo kutakaswa. Pia unaweza kutakaswa pasipo kujazwa Roho Mtakatifu. Tumelihakikisha kwa taratibu za asili.

Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni nini? Ni Roho anapokubatiza na kukuingiza ndani ya mwili wa Yesu Kristo (IKor 12:13). Ni kuzaliwa upya. Ni Roho wa Mungu anapoingia ndani na kukujaza baada ya kutubu (Baada ya kusikia neno) na kubatizwa katika maji kama jibu la dhamira safi mbele za Mungu (Mat. 2:38).

Kama u mbegu, halisi utalisikia neno; Roho atakubatiza na kukuingiza ndani ya mwili wa Yesu Kristo, Anakujaza na kukutia nguvu, na unalipokea Neno la siku na wakati wako
(IThes 1:2-6).

Na pia kuzaliwa upya ni machafuko. Amen. Inakufanya wewe kufanya vitu ambavyo hukufikiri kufanya, unasimama kwenye kona na kupiga ngoma au kuimba, utukufu kwako Mungu, Haleluya, utukufu kwa Mungu kwa nini unafanya kama mwenda wazimu.

Hicho ndicho kilichofanyika kwa wanafunzi, hilo ndilo lililofanyika kwa Bikira Maria, alitenda kama aliyelewa. Alikuwa uchafuko kwa jamii, lakini inachukua uchafuko kwa maisha mapya kudhihirika nje yake Amen. Mpaka kitu chochote kife na kuoza uhai hauwezi kutoka ndani yake mpaka mtu afe na kuoza katika fikira zake - Kristo hawezi kuingia katika moyo huo. Wakati unapojaribu kufikiri wewe mwenyewe "sasa kama nitatembea mpaka kwenye madhabahu na kusema ndiyo, Bwana ni mshirika mwema, ninakukubali wewe nitalipa zaka zangu", nitafanya hivi" unapaswa kufa na kuoza pale kwenye fikira zako. Acha Roho Mtakatifu achukue nafasi na kufanya vyovyote anavyotaka kufanya ndani yako. Iwe kama ni mchafuko ndio uwe mpole, hiyo inaonekana kwamba ni ya kutisha, siyo mbaya sana, lakini ni ya ukweli ndio njia pekee ninayojua kuliweka ili kukufanya ulielewe hilo.

Ninakwenda kusema kitu fulani, na ninataka kizame ndani, na Mungu anisaidie. Kuna upande wa misisimko inayoitwa Roho Mtakatifu leo katika makanisa hawalijali neno. Wanajijenga kwa wingi na misimamo ya kidini, wanakimbia mbali na hapo, kwa sababu hawalijali neno. Wanakwenda tu pamoja "Oh", tuna mikutano mikubwa. Halleluyah Halleluyah, halleluya.

Sasa wakati unafanya hivi, na hutoi matunda ya Roho, hapo unakufa katika roho mpya. Hukuwa ukifanya hilo, hiyo ni kweli. Lakini Mungu atakupatia wewe Roho mpya (Zab 51:10-11) kwa nini, roho uliyokuwa nayo hukuweza kupatana nayo mwenyewe? Sasa iwezekaneje mbele za Mungu?

Kwa hiyo Mungu anakupa wewe moyo mpya, sio uliowekwa viraka moyo mpya. Hiyo ni akili yako unayofikiri nayo njia mpya ya kufikiri. Wakati huo unapopewa njia mpya ya kufikiri. Ndio hilo nisawa, Biblia inaonekana na ndiyo ni sahihi. Nilikuwa nimezoea kutoamini hilo, ninaliamini sasa, sasa huo ndio uamsho wako mkubwa. Unaona?

Wanasema, "Ndio kweli, hatupendi kwenda kuzimu. Ninataka kumkubali Kristo". Hilo ni kweli. Nivema. Huo ndio mwanzo wako…….?

Tena Anasema baada ya hilo "Nitakupa roho mpya" Hiyo ni nini? Shauku mpya, "Nataka kufanya kitu sahihi" Sasa ninajua ni mkristo, nimelipata hilo ….. Ninavuta mara moja tu na kutupilia mbali, ninabaki nyumbani usiku, na unajua nita ……… nita hizo ndogo hiyo ni sawa ……. Hawa alisimama kwa muda kidogo tu. Hayo ndiyo aliyofanya.

Lakini sasa, hiyo ni roho mpya, wakati huo angalia utaratibu wa maandiko, Baada ya kupata moyo mpya na roho mpya, Anasema nitakupa Roho yangu… Unaona? Oh nini? Hayo ndiyo maandiko yanavyosema hapo. Huo ndio utaratibu tarakimu taratibu za hesabu za maandiko, moyo mpya, roho mpya, na Roho yangu (Ezekiel 36:24-29).

Moyo mpya wa Mungu unaingia ndani yako, anauweka katikati yako. Hapo ndipo nguvu zako za uendeshaji zinapoanzia kukuongoza. Na Roho mpya inajipanga katikati kabisa ya moyo mpya. Na Roho wa Mungu, Roho Mtakatifu anajipanga katikati kabisa ya Roho mpya. Na hapo ndiyo utawala wa mwenendo wako unafanyikia.

Lakini kuna kanisa moja tu na kuna njia moja tu ya kuingia ndani yake na hiyo ni kwa kuzaliwa. Unazaliwa ndani ya Kanisa la Yesu Kristo na kuwa mmoja wao ndani ya mwili wake, na kuwa mgeni wa kiroho wa mbinguni. Na ishara za kwamba Kristo yupo na wewe zinaonekana zikiishi ndani yako.

Wakristo, Oh, lazima uwe na mahusiano ya kibinafsi na Mungu. Ili kuwa Mwana wa Mungu, ni lazima uhusiane na Mungu. Ni lazima awe Baba yako na wewe uwe Mwana. Na ndio tu wanae wakiume na wakike wa Mungu ndio watakaookoka. Sio wanakanisa lakini wana na mabinti. Kuna kitu kimoja kinachoweza kufanya hilo ni kuzaliwa upya. Kuzaliwa upya ndio pekee kunakoleta mahusiano kati yako na Mungu. Hiyo ni kweli? Wana na mabinti…………

Wakati hili linapotendeka "Sasa tutafanya nini tena wakati tumezaliwa mara ya pili? Wengi wameniuliza swali hilo vipi nitafanyaje sasa Ndugu Branham?" Kama umezaliwa mara ya pili, tayari asili yako yote imebadilika kabisa, umekufa kabisa na vitu vyako ulivyokuwa ukiwaza kabla.

"Vema" unasema ndugu Branham nilipojiunga na kanisa nililipata hilo. Vema wakati Mungu alisema Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na milele; anaendelea kuponya wagonjwa, anaendelea kuonyesha maono. Lakini Ndugu Branham, Kanisa langu …." Sasa hujazaliwa mara ya pili. unaona? Huwezi kuwa, kwa maana kama Mungu yule, kama uhai wake uko ndani yako, kama wewe uhai wako kwa Baba yako na uhai halisi wa Mungu upo ndani yako na Roho yule aliyekuwa kwa Kristo yuko ndani kwako. Iweje Roho aliyekuwa ndani ya Kristo aandike hilo na tena aje ndani yako chini yako na alikatae hilo? Ona? Huwezi kufanya hilo. Inalikubali kila neno kwamba ni hivyo.

Wakati hilo linapotendeka kitu utakachokifanya sasa, Roho anayekuja kwako kutokana na kuzaliwa upya. Utaamini na kufanya kila kitu ambacho Mungu amesema katika neno lake wewe ukifanye. Na kila kitu ambacho Biblia imekisema kwa ajili yako. Kukifanya, utakikubali na kusema "Amen". Hutasimama usiku na mchana mpaka ukipokee. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli na kwa muda wote kwa uhakika juu ya kila kitu utazaa tunda la Roho (Gal. 5:22).

Unasema "nitanena kwa lugha?" Unaweza kufanya hivyo, na unaweza usifanye hivyo "nitapiga kelele, unaweza kufanya hivyo au hapana. Lakini kuna kitu cha kweli utafanya utazaa tunda la Roho, na tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, imani, upole, kiasi, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, subira, hasira zako haziwezi kuwa ……… kumbuka unapopata hilo. Hilo ni sumu kwa Roho Mtakatifu anakuwa mbali nawe. Ona? Wakati unapokuwa mahali ambapo unapenda kuzoza na kila mtu unayekutana naye, ujue kuna kitu siyo sahihi.

Unapofika mahali ambapo mhudumu anasoma kutoka kwenye Biblia kwamba ni kosa kufanya kitu fulani, nawe hukubaliani nacho ukumbuke hakuna ukristo hapo utawajua, kwa matunda yao. Ni vile Yesu alivyosema (Mat. 7:15-20).

Kama ni Neno na Mungu amelinena, Roho aliye ndani yako atakubaliana nalo kila wakati. Kwa sababu Roho Mtakatifu halisi anakubaliana na kila neno 'Kwa sababu Neno ni Uzima na Roho, Yesu alisema Neno langu ni Uzima (Yoh. 6:63) Na kama unao Uzima wa Milele, naye Ni Neno. Jinsi gani Neno likane Neno? Ona? Utamfanya Mungu awe ni mtu wa namna gani? Kitu kimoja unachoweza kufahamu kuwa wewe ni Mkristo. Ni wakati wewe unapokubaliana na kuamini kila Neno la Mungu, na utajikuta unawapenda maadui zako (Math 5:43-48).
Mtu mmoja anasema "vema yule si kitu ila Mtakatifu anayevingirika na unaanza kupata …….. Oh uwe mwangalifu, uwe mwangalifu. Lakini unapojiona mwenyewe kwamba unampenda, kweli usijali ni kitu gani wanafanya, wewe endelea tu kuwapenda. Halafu unaanza kujua ……………..

Na subira yako inatakiwa kwa muda mrefu bila kuangalia mwisho. Mwingine anasema kitu kuhusu hilo, "Vema usijali anasema nini ….." Usianze kujisikia na kuchochewa, kama unaona kuchochewa ni vema ukiomba kwanza kabla ya kuwa na mazungumzo nao zaidi Ona? Ndio. Lisiingie kwenye kuzoza. Usipende kuingia kwenye mizozo kama unataka kuona mmoja akisimama ndani ya Kanisa na kusema "Unajua nini? Ninakuambia fulani na fulani, alifanya lile na lile" sema, Ndugu aibu kwako. Na kama utasema 'Oh, ndio hivyo? Unasikiliza jambo hilo la aibu Angalia Roho Mtakatifu sio jalala "Ona? Hapana, hapana, hapana.

Moyo uliokaliwa na Roho Mtakatifu umejaa utakatifu, usafi haufikirii maovu, haufanyi maovu, huamini yote, huvumilia, huwa na subira.
Usizoze, wakati jamaa inapoingia kwenye mizozo, usiingie pamoja nao. Sasa usizoze unaona? Hasira huzaa hasira, Jambo la kwanza utamhuzunisha Roho mtakatifu nawe utaanza kuzoza. Ndipo Roho Mtakatifu anapoondoka, hiyo ni kweli. Hasira huzaa hasira na upendo huzaa upendo. Ujae upendo. Yesu alisema watu watajua kwamba ninyi ni wanafunzi wangu mkipendana ninyi kwa ninyi. Hilo ndilo tunda la Roho Mtakatifu – upendo (Yoh.13:34-35).

Je unafahamu kwamba wewe mwenyewe ni muumbaji mdogo? Ulifahamu hilo? Hakika. Umeona watu ambao unapenda kuwa karibu nao, hujui ni kwa nini, wale watu wenye upendo. Hujaona hilo? Ni wakarimu kadiri inavyoweza kuwa, unapenda kuwa karibu nao. Wanaumba mazingira hayo kwa maisha wanayoishi. Namna wanayozungumza, majadiliano yao. Halafu umeona wale ambao kila mara usingependa kuwa karibu nao. Wakati wote wanataka kuzungumzia kitu fulani kiovu, na kumsengenya mtu fulani, na kusema "Oh, jamani, wale wanakuja, wataenda kumshutumu mtu fulani. Yupo hapa sasa, ataenda kuzungumza juu ya mtu yule. Yote wanayoenda kufanya nikuzungumza mizaha michafu, au jambo fulani juu ya wanawake, au kitu kama hicho" Unachukia tu kuwa karibu nao. Unaona? Wanaumba. Wanaonekana ni watu wazuri, lakini wanaumba yale mazingira. Na mambo yale unayofikiria, mambo yale unayotenda, matendo, mambo unayozungumzia yanaumba mazingira. …………

Acha nione kile unachotazama, kile unachosoma na aina ya muziki unaosikiliza, makundi unayojumuika nayo, na nitakuambia ni roho gani iko ndani yako. Una ona? Ndiyo.

Utasikia mtu akisema mimi nimefanya hiki na kile? Hilo kundi la" …… Sasa Kumbuka, sijali anavyosema matendo yake yanasema kwa sauti kuliko chochote anachoweza kusema. Anaweza kujishuhudia, akisema ni Mkristo (kweli) na anaweza kufanya kitu chochote. Lakini angalia aina ya maisha anayoishi. Hiyo itakuonyesha jinsi alivyo.

Ngoja nikuambie. Hakika usijaribu kujiunga na Kanisa sasa. Hilo halisaidii kitu 'uzaliwe mara ya pili, sio misisimko inayofanya kazi; sio kitu kidogo ulichosema " Vema, nimepiga makelele, Nimenena kwa lugha, nafanya kile na kile au kile". Ni kule kwenye kilindi cha moyo wako. Kitu fulani kinakuja kukubadilisha nawe

Unakuwa kiumbe kipya katika Yesu Kristo. Unaupokea utu wa Kristo Yesu, wakati mambo ya kale yamekufa kabisa, na vitu vipya vinazaliwa tena unafanya mambo yote sahihi ambayo, kwamba uliyafanya kimakosa unawapenda maadui, zako unawaombea wale wanaokuudhi. Hapo ndipo sasa umkristo. Mti hufahamika kwa matunda yake unayozaa.

Katika Yoh. 12:20 –25 tunaona Wayahudi walitaka kumwona Yesu. Hawakumwona kwenye Krismas, hawakumwona kwenye madhehebu yoyote hawakumuona kwenye kanuni za imani zao, Hakuwaelekeza kamwe katika hayo. Umelipata vema hilo? Lakini aliwaelekeza msalabani ili kufa, kufa. Wanafunzi wa kweli husema yakupasa "ufe" nitajuaje kwamba nimekufa? unapolikubali neno hili lote kwamba ni Kweli. Hapo neno linaanza kuishi ndani yako.

Kama Yesu alivyosema, mara ukubalipo hili Neno. Hili neno litajidhihirisha ndani yako. Litafanya sawa sawa kama lilivyosema, litafanya ndani yako.

Oh, wengine wengi leo wanajaribu wenyewe kujijengea wazo lao. Nimepata njia yangu, juu ya hilo ninaiamini, hiyo lakini huwezi kumpata Kristo mpaka kwanza ufe mwenyewe na kumkubali yeye, Neno, hapo utaona uzima.

Kwa hiyo Yesu alisema lazima uzaliwe mara ya pili, ile kuzaliwa mara ya pili, nikujiondoa njiani wewe mwenyewe ufe, na Roho wa Kristo atakuja ndani yako. Sasa sio wewe tena bali ni Kristo ndani yako, Roho Mtakatifu. Paulo alisema. Ninakufa kila siku 1Kor. 15:31) Bado ninaishi, sio mimi, ila Kristo anaishi ndani yangu Gal. 2:19 – 20) Unaona, Kristo ………….

Sasa, wanasema "ukishika dini sana itakufanya mwendawazimu. Vitu vingi vibaya vinakufanya mwendawazimu. Lakini dini ya Yesu Kristo, Kama umwendawazimu inakuweka kwenye akili timamu Unaona? Huwezi kuwa sahihi mpaka uzaliwe mara ya pili. Huko na bongo safi mpaka uzaliwe mara ya pili. Mtu hawezi kuwa katika hali nzuri mpaka azaliwa mara ya pili. Ni mnyama moyoni – mpaka azaliwe na Roho wa Mungu, na roho wa asili anatolewa nje yako, na Roho wa Mungu anachukua nafasi ya kutawala. Kwamba anakuongoza, na kukuelekeza katika kweli na Nuru. Hiyo ni kweli na kama mtu hatafanya hilo, Naye anajua pasipo hilo kuzimu inamngojea, kuna kitu kisichosahihi kwenye bongo yake. Kwa nini, watu hawapendi kulipokea hilo? Kwa nini?

Wanakataa kupokea au kuchukua dawa ya daktari, kuzaliwa upya.

Sasa walimu wa uongo wanaleta kuzaliwa kwa uongo, Nabii wa kweli analeta Neno, kuzaliwa na neno, Kristo. Nabii wa uongo analeta kuzaliwa kwa uongo, kuzaliwa na kanisa, kuzaliwa na kanuni za imani, kuzaliwa na madhehebu, na hapo unasimama umpetekoste Ndugu msisimko wa uongo, nakumuambia mtu umempata Roho Mtakatifu, sababu amenena kwa lugha. Nimeona mashetani yakinena kwa lugha. Kalamu ikiwekwa na kuandika lugha isiyojulikana. Hivyo siyo kitu haimaanishi kitu. Unaona, Inapasa iwe ni maisha, kwa matunda yao mtawatambua. Ndugu Branham unaamini kunena kwa lugha? Ndio Bwana, unaamini kupiga makelele? Ndio Bwana kuwa Mkristo, ninaamini hilo. Ninaamini Neno la Mungu. Lakini kama maisha yako hayaendi sawa na hilo.

Toka kwenye joho la Bandia "utukufu kwa Mungu haleluya. Na uniambie kwamba hilo ni Kristo. Kristo ni mnyenyekevu, mpole,na mtulivu.

Na sikiliza, Sasa ninasema kitu fulani hapa, nataka msikilize. Kuna mafundisho haya ya uongo. Aina ya dhana za uongo (unajua mafundisho ya uongo ni nini?) yameongoza mamilioni ya watu kwenye kuzaliwa kwa uongo. Walimu wa uongo wanaongoza watu kuamini misisimko." Sababu umetikiswa mwili wote umempata Oh, kwa sababu umepata mguso wa ajabu, umeona mwanga mbele yako, umepata upofu na kupapasa. Hilo ni Koti la Eliya umevishwa. Hiyo ni kweli, umelipata hilo, Oh, unajua mahali ulipo, mwana wa Mungu, aliyedhihirishwa utajikuta wapi mwenyewe? Aliyeshindwa. Hiyo ni kweli, utukufu kwa Mungu, usiku mmoja niliota ndoto oh, ndio oh, nimeona hilo kwamba …………. Ndio Je huamini ndoto? Oh, Ndio ninaamini. Lakini kama ndoto hiyo hailingani na neno la Mungu hiyo ni kosa. Hii ni kweli hapa, kaa kwenye hilo, ndio, Bwana. Linaongoza mamilioni ya watu kwenye kuzaliwa kwa uongo hebu fikiri …………

Kama umezaliwa na Mungu umeoshwa katika maji ya Neno Efeso 5:25 – 27) umetengwa na vitu vya dunia, na kumwamini Mungu. Umekufa, umekufa katika mawazo yako, ufe katika mawazo yako, Umekufa katika kila kitu isipokuwa Neno la Mungu (Kol.3:14) litaishi ndani yako, linafanya kazi kupitia wewe, likithibitisha kwamba ni Neno la Mungu. Unasema, "Nimekufa kwenye mambo ya ulimwengu, nimekufa na ulimwengu Ndugu Branham "Na unakana neno la Mungu?.

Yesu alisema, ishara hizi zitaambatana na hao waaminio. Sasa tunaenda kuelewa nini maana ya kuzaliwa mara ya pili Unaona?

Bado una hasira, bado mchoyo, kiburi, mtu mwingine anasema kitu kingine kuhusu wewe, tayari unataka kupigana, wakati huo umezaliwa na Roho wa Mungu? Hapana, Roho wa Mungu hafanyi hivyo, hapana. Roho wa Mungu ni mnyenyekevu, mpole mwema, mvumilivu. Huyo ni Mungu mwenye Upendo, mkarimu, msamehevu. Huyo ni Roho wa Mungu Oh, ndio.

Lakini wanaoshikilia madhehebu hayo na wananena kwa lugha, wanatabiri wanafanya kila aina ya kazi. Yesu alisema watafanya hivyo, wenye mfano wa utauwa (IITimo 3:1-5) Wanashikilia madhehebu kwa sababu ndio baba yao, wamezaliwa na baba yao madhehebu, lakini kama umezaliwa na Mungu. Huyo ndio Baba yako, yeye ni neno, Neno, Haijalishi ni misisimko ya kiasi gani umepata; bado ni mtoto wa shetani mpaka ufe kwa ulimwengu na uishi kwa ajili ya Kristo.

Nafsi njema au mbaya kifo hakiibadilishi. Ninayo maandiko mengi yaliyoandikwa hapa juu ya hili moja ninalotaka kutolea hoja ni Nafsi ni nini? Wewe ni nafsi, sehemu ya ndani yako, na utakapokufa, Daima nafsi ilivyo ndivyo itakavyokwenda. Itakwenda kwenye makao yake. Huwezi kuirudisha tena juu japo ufanye nini juu yake. Hivyo nafsi lazima kubadilishwa hapa, kuzaliwa mara ya pili.

Usijaribu kuwa na msisimko au kitu chochote kuchukua nafasi ya Roho Mtakatifu. Wakati kuzaliwa mara ya pili kunapokuja unabadilika tu. Huhitaji kufanya kitu chochote kuhakikisha hilo. Maisha yako yataonyesha hilo. Kadiri unavyotembea upendo wako, amani, utu wema, "uvumilivu, upole subira. Hivyo ndivyo ulivyo na ulimwengu wote utamwona Kristo kupitia wewe.

Sasa kunena kwa lugha, kupiga makelele, hayo ni matokeo tu ambayo yanafuatana na hayo maisha na unaweza kuigiza tu hayo matokeo ya hayo maisha na bado huna hayo maisha hakika mnajua unaona hilo. Ni wangapi wanaojua hilo ni kweli? Oh, Jamani, utaliona hilo kote.

Kwa hiyo hakuna kitu unachoweza kusema ni ushahidi wa Roho Mtakatifu mpaka maisha yako unayoishi. Kama unataka kunena kwa lugha, hiyo ni sawa sawa kabisa, kama maisha yanakuwa sawa sawa na hilo. Hiyo ni sawa. Na kama unataka kupiga makelele, vema, hilo ni zuri. Ninapiga kelele, mno, ninakuwa na furaha mara nyingi nashindwa hata kuvaa viatu, napenda kuruka, nitoke ndani yake hayo ni maajabu. Naamini hilo.


Nukuu za kiingereza :
Uchungu wa kuzaa, uk. 13,27
Elimu juu ya mapepo – milki ya kidini Aya 56-57
Mbegu haitarithi pamoja na kapi (65 – 0218) Aya 48-50
Kitabu cha nyakati saba za Kanisa Smirna Uk. 154/Effesso Uk. 96 –97
Uigizaji wa ukristo aya 110-114
Je maisha yako yanastahili Injili Aya 137 –153
Ndipo macho yao yakafumbuliwa Aya 137-153
Mabwana tunataka kumuona Yesu Uk. 15+30
Uinjilisti wa wakati wa mwisho Aya 57
Kwanini (60-0309) Aya 19/Lazima kuzaliwa mara ya pili Aya 129-131, 107-111



Jiwe la kujengea la kiroho nambari 132 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, yamekusanywa na Gerd rodewald friendestr.69,D-75328 Schomberge Germany simu (+49) 72357613 Fax 72353306.


Amekuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia [Nd. Branham katika mwenendo, utaratibu na mafundisho Uk. 724]

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*


*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*